KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 19, Issue 3

25th Rabiul Awwal 1433

17th Feb, 2012

HUKMU YA ISBAAL KATIKA UISLAMU

Na: DR. SALEH AS-SALEH

NI NINI ISBAAL?

Isbaal ni kuvaa nguo ndefu zinazopita (au kuvuka) chini ya vifundo vya miguu.

KWANI IMEHARAMISHWA?

Naam, ndio! kwa sababu amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "*Sehemu ya Izaar (nguo) inayovuka chini ya vifundo vya miguu ni ya motoni."* [swaheeh al-Bukhaari, V.7, hadeeth # 678].
Baadhi ya watu wameshikilia rai yakwamba *Isbaal* imeharamishwa pindi itakapokuwa imefanywa kwa majivuno, kiburi au kujitwaza. Jee, hoja hii ina ukweli?
Laa, si kweli kwa sababu:

KWANZA: Tishio la kuadhibiwa kwenye moto wa Jahannam wenye kuburuta nguo zao chini ya vifundo vya miguu ni jambo la wazi kabisa. Sehemu itakayostahiki adhabu ni ile yenye kuikhalifu amri ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), yaani chini ya vifundo vya miguu. Al-Haafidh ibn Hajar ni miongoni mwa wenye rai yakwamba maana ya dhahiri ya hadeeth hiyo ndio ukweli ulivyo. Yaani, nguo pamoja na sehemu iliyo chini ya vifundo vya miguu zitakuwa kwenye moto kama ilivyo hali katika maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى): **"Hakika nyinyi (makafiri) na wale mnaowaabudu hivi sasa, mkamuacha Allaah, ni kuni za Jahannam."** (al-Anbiyaa' 21:98).
Angalia kwenye fat-hul-Baari V.10, hadeeth # 5789 (iliyo sawa na # 678 hapo juu) Uk. 268-269, Iliyochapishwa na *Daar ar-Rayyaan, Cairo, Egypt.*

PILI: Maandiko mingi sana yanaashiriya yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiwaamrisha watu wapandishe juu nguo zao. Wanavyuoni wengi wa ki-Islamu (Al-Jamhoor) wameafikiana yakwamba iwapo maandiko yanapokuwa katika hali ya kuamrishwa, basi inakuwa imekusudiwa *Tahreem* (kuharamishwa), isipokuwa kutakuwa na ushahidi mwengine ulio swaheeh wenye kuashiriya vyenginevyo. Katika tukio fulani, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimuona mtu mmoja akiburuta nguo zake (vazi lake la chini), akamfuata kwa haraka na kumwambia: *"**Pandisha ju u** Izaar yako na umche Allaah."* Yule bwana akasema: "Mimi ni mtu 'ahnaf', mwenye kutetema magoti [Ahnaf ni mtu mwenye maradhi ya kutetema magoti yakawa yanagusana kuanzia kwenye dole gumba]. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: *"**Pandisha juu** Izaar yako! Kwa hakika, kila alichoumba Allaah ni kizuri."* Basi kuanzia hapo mtu huyo hakuwahi kuonekana isipokuwa alikuwa amevaa Izaar iliyogusa katikati ya miundi yake ya miguu au mpaka katikati ya miundi yake ya miguu. [Imepokewa na Ahmad na wengineo, na inatosheleza masharti na riwaya zilizowekwa na al-Bukhari na Muslim. Tizama katika as-Silsila as-Swaheehah # 1441]
Hapa inaonyesha wazi yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakumuuliza huyu mtu iwapo alikuwa akifanya kitendo hicho kutokana na kiburi au kujitwaza. Kwa hakika ni dhahiri yakwamba kutokana na hali aliyokuwa nayo mtu huyo ni kwamba hata hakuwa na fikra za majivuno! Licha ya hayo yote, Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakumkubalia *isbaal* yake na akayazingatia yote hayo kwenda kinyume na *at-Taqwaa* (Ucha Mungu).

TATU: Makatazo ya ki-Ujumla ya Isbaal yako wazi kulingana na hadeeth za Mtume (صلى الله عليه وسلم). Wakati mmoja alimwambia Sufyaan Bin Sahl: *"Ewe Sufyaan Bin Sahl! **Usishushe** nguo yako chini ya vifundo vya miguu kwa sababu Allaah hawapendi Musbileen (wenye kushusha nguo zao za chini kupita vifundo vyao vya miguu)."* [Swaheeh Sunan ibn Maajah cha Sheikh Naasir ud-Deen al-Albaani # 2876].
Jaabir bin Saleem amesema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwambia: *"... **Na ujitahadhari** na Isbaal ya Izaar kwa sababu inatokamana na Al-Makheelah (*majivuno, kiburi au kujitwaza*) na Allaah hayapendi hayo."* [Silsilat al-ahaadeeth as-swaheehah, mfululizo juu ya ukusanyaji wa ahaadeeth zilizo swaheeh, na Sheikh al-Albaani #770]. Imebainika kwa kila mtu yakwamba maandiko yaliyopigwa mstari yameandikwa kwa njia ya kuamrishwa, na huko ni kuashiriya makatazo ya *Isbaal*, yawe yametekelezwa kwa njia ya Makheelah au laa. Al-Haafidh Ibn Hajar, katika uchambuzi wake kuhusiana na baadhi ya ahaadeeth zilizotangulia kutajwa, amesema, "Isbaal iliyotajwa kwenye ahaadeeth hizi ni katika madhambi makubwa iwapo yatafanywa kwa njia ya Makheelah, vyenginevyo ni kwamba maana iliyo dhahiri ya ahaadeeth hizo inaashiriya yakwamba yamekatazwa." [Fat-hul-Baari V.10, Uk. 263].

NNE: Ubainifu wa Aya isemayo: **"Na anachokupeni Mtume basi pokeeni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho."** [Al-Hashr 59:7]. Ni jambo lijulikanalo yakwamba "Thawb" (nguo) ya aliyekuwa akiheshimiwa mno miongoni mwa wana-adamu, Muhammad (صلى الله عليه وسلم), "كان ثوبه إلى نصف ساقيه" ilikuwa ni mpaka katikati ya miundi yake." [Imepokewa na Ahmad, at-Tirmidhee katika ash-Shamaa'il Al-Muhammadiyyah na wengineo. Hadeeth hiyo ni swaheeh kama ilivyopokewa na Waleed an-Nasr katika kitabu chake Al-Isbaal Lighayr

YALIYOMO

HUKMU KUHUSU ISBAAL 1 - 4

al-Khuyalaa', Uk. 15, Chapa ya pili, 1411/1990 (jina la mchapishaji halikutajwa)].
Limethibitishwa hili kwenye hadeeth ambayo 'Uthmaan (رضي الله عنه) amepokea yakwamba *"Nguo ya chini ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) imefikia katikati ya vifundo vyake vya miguu."* [Imepokewa na at-Tirmidhee katika ash-Shamaa'il Al-Muhammadiyyah na Sheikh al-Albaani akaiswahihisha # 98]
Sasa ni yupi huyo alo na unyenyekevu kuliko Mtume (صلى الله عليه وسلم)? Alikuwa akijua yakwamba Isbaal hushurutisha *Al -Makheelah* hata kama musbil mwenyewe hakukusudia hayo. Hili limeungwa mkono na hadeeth ya Jaabir Bin Saleem, pindi Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipobainisha yakwamba **Isbaal ni ubainifu wa kibri:**
Alimuamrisha Jaabir bin Saleem kwa kumwambia: *"Na upandishe Izaar yako mpaka katikati ya miundi yako, na iwapo hupendi hivyo, basi mpaka kwenye vifundo viwili vya miguu yako (yaani; mpaka ufikie juu ya visigino)* ***<u>na ujitahadhari na Isbaal kwa sababu (huko ni kujitwaza).</u>"*** [Silsilat ahaadeeth as-Swaheehah, hadeeth # 1109 na 1352]
Kwahivyo haimpasi mtu kuifuata amri itokayo kwa Allaah katika aya hiyo iliyotangulia?

<u>TANO:</u> Wanaume wenye kuvaa Isbaal wanajifananisha na Wanawake.
Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwakataza wanaume wasivae nguo kama wanawake na kinyume chake.
Akasema: *"Allaah amemlaani mwanamume aliyevaa kama mwanamke na mwanamke aliyevaa kama mwanamume."*
Kwa kweli, Ibn 'Umar (رضي الله عنهما) amesema yakwamba: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema, 'Mwenye kuburuta nguo yake kwa majivuno, Allaah hatomwangalia katika Siku ya Malipo.'"Umm Salamah (رضي الله عنهما) amesema: "Yaa Rasoolullaah, sasa wanawake wafanyeje na ncha za chini za nguo zao?" Akamjibu: *"Wanaruhusiwa kuzidisha urefu kiasi cha msamba mmoja wa mkono."*
Akasema (Umm Salamah): "Hapo bado miguu yao haitokuwa imefichika."
Akamjibu tena: *"Basi na wazidishe urefu wa ncha za chini za nguo zao pima nzima, wala wasizidishe hapo."*

Kuzidisha urefu wa nguo chini ya visigino ni desturi za nguo za kike.
Amesema Shaykh Ul-Islaam Ibn Taymiyyah (رحمه الله): "... miongoni mwa mifumo ya kuwaiga (wengine) katika maumbile ya kudhihirika huleta dhana za uwiano kati ya matendo na desturi. Hiyo ndiyo sababu tukaonywa kuhusu kuwaiga *ma-Kuffaar* ... na hiyo pia ndiyo sababu ya kwanini wanaume na wanawake wakakatazwa kuigana kwa kila kitu katika hadeeth isemayo: *"Mwenye kushabihiyana na watu fulani huwa ni katika wao.."*
Mwanamume mwenye kuwaiga wanawake hupata kuiga kutokamana na tabia zao kulingana na kiwango anachoiga, kiasi cha kwamba hwenda akamalizikia na tabia za kike tupu.
Mwanamke anayewaiga wanaume huchukuwa sehemu za tabia zao mpaka afikie viwango vya *Tabarruj (kujionyesha mapambo yake kwa wasiomuhusu), Burooz (kujionyesha mbele ya watu) na Mushaarakah (kujishirikisha na wanaume katika kila nyanja)*, na wanaume wakawapelekea baadhi yao waonyeshe miili yao kama wafanyavyo wanaume, wakidai ubora kuliko wanaume, na wakafanya kila lenye kukhalifu haya za mwanamke.
'Umar Ibn al-Khattab (رضي الله عنه) alipomuona mtu mmoja akiburuta *Izaar* yake, alimwita akamwambia: "Wewe uko katika heidh?" yule mtu akajibu: "Ewe Ameer Al-Mu'mineen! Mwanamume pia huingia kwenye heidh?" 'Umar akamwambia: "Kwani ni jambo gani lililokufanya wewe uburute *Izaar* yako kupita vifundo vya miguu yako?" kisha akaamrisha kuletwe wembe, akakunja (sehemu za ncha za nguo) za Izaar ya yule bwana na akakata kilichozidi kupita vifundo vya miguu.
Leo sisi twawaona watu wakiburuta *Izaar* zao (Thawb, surwale ndefu, surwale fupi, n.k) kama wanawake, haliyakuwa wanawake wanavaa nguo ambazo ncha zake za chini ziko juu juu ya visigino vyao! Twamuomba Allaah awaongoze waume wetu na wake wetu washikamane na amri za Allaah na Mtume wake (صلى الله عليه وسلم).

<u>SITA:</u> ***Isbaal ni israfu:***
Allaah ameweka vipimo katika kila kitu, zikiwemo nguo za wanaume. Muislamu anapozidisha viwango vilivyowekwa na Sheriya, basi huwa amefanya israfu.
Amesema Allaah (سبحانه وتعالى) [kama ilivyofasiriwa: **"Na kuleni (vizuri) na kunyweni (vizuri). Lakini msipite kiasi tu. Hakika Yeye (Allaah) hawapendi wapitao kiasi (wapindukiyao mipaka)"** [Al-A'raaf 7:31]
Al-Haafidh Ibn Hajar (رحمه الله) amesema: "Iwapo *Thawb* (na vilevile nguo za aina yoyote) itazidi kipimo chake cha sawa cha mwenye kuivaa, basi na ikatazwe kwa kutegemezwa juu ya mlango wa israfu na hilo hupelekea kwenye *Tahreem."* [Fat-hul-Baari V.10, Uk. 263].

<u>SABA:</u> **Isbaal ni Uchafu**
Amesema 'Ubayd Bin Khaalid: "Siku moja nilikuwa nikitembea na huku naburuta *Burd* langu (Nguo kubwa nyeusi ya mapambo). Akawa mtu mmoja nyuma yangu ananiambia: "Pandisha nguo yako juu, kwa sababu kufanya hivyo (kutaiweka nguo yako) iwe safi na itadumu." nikageuka (ili nimuone ni nani huyo anaezungumza na mimi), akawa si mwengine bali ni Mtume (صلى الله عليه وسلم).
Nikamwambia: "Ni *Burdah* (nguo ya juu) yenye nyuzi nyeupe na nyeusi tu." Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia 'Ubayd Bin Khaalid: "*Kwani wewe huna mfano bora kutoka kwangu mimi?"* Nikamjibu: "Nikamwangalia na nikaiona urefu wa Izaar yake imefikia katikati ya miundi yake."
Abdullaah Ibn Mas'ud amesimulia yakwamba: "Kijana mmoja alikwenda kumtembelea 'Umar (رضي الله عنه) [baada ya kudungwa kisu na Abu Lu'lu'ah Al-Majoosi] akaanza kumsifu 'Umar (رضي الله عنه). (Mpokezi wa athar hii) akasema: "'Umar akamuona yule kijana anaburuta Izaar yake."
Akamwambia: "Ewe kijana cha ndugu yangu! Pandisha nguo yako juu, kwani huko kuipandisha kutaiweka nguo yako kuwa safi, na kukuokoa wewe na adhabu ya *Rabb* (Mola) wako."
Maafa ya uchungu yaliyotokamana na vyembe vilivyomuathiri 'Umar hayakumzuiya 'Umar kuzungumza kuhusu mas'ala ya *Isbaal* kwa sababu 'Umar alifahamu vitisho vya adhabu ya Moto kwa wenye kuburuta nguo zao za chini. Katika haya kuna mafunzo makubwa kwa Waislamu wote na hususan kizazi chetu cha vijana yakwamba wayachukulie mas'ala haya kuwa na umuhimu mkubwa na washikamane na amri za Allaah na Mtume wake (صلى الله عليه وسلم).
Kwa upande mwengine, tukio hili laonyesha yakwamba 'Umar, kama kiongozi wa Ummah, hakuliona jambo hili kuwa ni mas'ala madogo, kama wanavyojibu baadhi ya Waislamu pindi wanapopewa naswiha kuhusu suala mfano wa Isbaal au kuweka Ndevu.
Aliyazingatia mas'ala yote ya Deen kwa muangaza wa mafunzo ya Qur'an na Sunnah. Hapana shaka yakwamba, ikiwa mtu ni mpya katika Uislamu au

awapo ni mjinga (hajui), basi kwa utaratibu tunaanza kumfundisha umuhimu wa Tawheed na kwamba Sunnah ni katika sehemu muhimu ya Tawheed. Atakapobainishiwa haya, basi ni jambo la kawaida kabisa kumlingania ashikamane nazo. Kuwa na mipango ya kupaumbele bila ya kulegeza misimamo au kuakhirisha kusikokuwa na mwisho, *insha-Allaah*, ndio njia ya kufaidisha.

TANBEEH: Huenda mtu akauliza suali: "Ikiwa Sunnah kwa wanawake ni kuburuta nguo zao, sasa jee, ni vipi kuhusu uchafu uwezao kubaki kwenye nguo zao hizo?"
Mwanamke mmoja alimuuliza Umm Salamah (رضي الله عنها) lifuatalo: "Mimi ni mwanamke ninayeburuta nguo yangu kutokana na urefu wake, na hupita kwenye njia zenye uchafu mwingi (sasa nifanyeje)?" Umm Salamah akamjibu: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: 'Kijacho baada ya uchafu huo, husafisha'."
Hadeeth hii imepokewa na Imaam Maalik, Ahmad, At-Tirmidhee, Abu Daawud na ad-Daarimee. Sheikh al-Albaani amesema yakwamba hadeeth hiyo ni swaheeh kwa vile imeungwa mkono na riwaya nyengine iliyo swaheeh iliyopokewa na Abu Daawud, ambapo mwanamke kutoka katika kabila la Banu Abd Al-Ashhal amesimulia: "Nilisema, Yaa Rasoolullaah! Njia yetu ya kuelekea msikitini ina uvundo (harufu mbaya); sasa sisi tufanyeje kunaponyesha? Akamuuliza: 'Kwani hakuna sehemu iliyo safi baada ya sehemu hiyo chafu ya barabara?' Akamjibu: 'ipo sehemu safi kwa kweli.; Akasema, 'basi hii (sehemu safi) inafidia hiyo (sehemu chafu).'" [Tizama kitabu cha at-Tabrizi *Mushkatul Masaabeeh, V.1, hadeeth # 504 na 512, iliyopitiwa na kusahihishwa na al-Albaani*].
Sharee'ah inamruhusu mwanamke aburute nguo yake ili awe amejihifadhi (amejifunika) miguu yake ambayo hayafai kuwachwa wazi mbele ya watu. Hii ni ruhusa inayomuhukumu mwanamke tafauti na mwanamume kuhusiana na kuburuta nguo.

UBAINIFU WA BAADHI ZA *SHUBUHAAT* KUHUSIANA NA *ISBAAL*

SHUB'HA YA KWANZA: *Isbaal* inaruhusiwa maadamu haifanywi kwa malengo ya *Makheelah*. Baadhi ya watu hurejea kwenye hadeeth ifuatayo kuwa ni dalili yao:
[Abdullaah bin 'Umar (رضي الله عنهما) amepokea yakwamba: "Nilikuja kumtembelea Mtume (صلى الله عليه وسلم) nami nikawa nimevaa Izaar *Yataqa'qa* (*ikitoa sauti ya kuburuta kutokana na uburutaji kupita chini ya vifundo vya miguu)*.Mtume (صلى الله عليه وسلم) akauliza: *"Nnani huyu?"* Nikamjibu: "Abdullaah bin 'Umar." Akasema: *"Ikiwa wewe ni 'Abd* (yaani; mtumwa wa kweli) *wa Allaah, basi pandisha juu Izaar yako."* Nikafanya hivyo. Kisha akasema, "Zaidi!" (Ibn 'Umar) akasema: "Nikaipandisha juu mpaka ikafika katikati ya miundi yangu: Huo ndio uliokuwa (urefu) wa Izaar yake (صلى الله عليه وسلم) mpaka kufa kwake."
Kisha akamwangalia Abu Bakr akasema: "Ikiwa mtu yoyote ataburuta nguo yake kwa majivuno, Allaah Hatomwangalia katika Siku ya Malipo." Kisha Abu Bakr akasema: "Mara nyengine Izaar yangu hushuka chini (katika riwaya nyengine alisema, "Upande mmoja wa nguo yangu ya chini hushuka iwapo siwi na tahadhari ya kuiangalia"). Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: "Lakini wewe si mmoja wao (katika riwaya nyengine, alisema: "Wewe si miongoni mwa wenye kufanya hivyo kwa majivuno")].

MAS'ALA: Hadeeth hii inaunga mkono kuhusu *Tahreem* ya (uharamu wa) Isbaal na wala si rai inayoruhusu Isbaal maadamu haikufanywa kutokana na majivuno. Kwa hakika, hadeeth waziwazi imefanya kuwa ni wajibu juu ya Muislamu asiwache *Izaar* yake kuwa ndefu zaidi na kupita vifundo vyake vya miguu, na kwamba ni lazima aipandishe juu hata kama niya yake ni kama ya Abu Bakr katika hadeeth hiyo, yaani; haikufanywa kutokana na majivuno. Kwa kweli Abu Bakr alisema: "Upande mmoja wa nguo yangu ya chini hushuka **iwapo siwi na tahadhari ya kuichunga.**"
Katika zama zetu, hatahivyo, **watu huziwacha Izaar zao zikishuka chini,** kinyume cha Abu Bakr, na kisha wakidai: "Aah, sisi hatufanyi hivyo kutokana na majivuno!" kwani wao hawazingatii yakuwa ni amri ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kupandisha juu Izaar zao na kwamba urefu wa Izaar yake ilikuwa ni mpaka katikati ya miundi yake? Kwani wao hawajui yakwamba yeye, Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakufikiria kuhusu Makheelah? Kwani yeye si mfano bora kwetu sisi?
Vilevile ni wazi yakwamba Abu Bakr hakuwahi kusema, "Mimi niliifanya Izaar yangu kuwa ndefu." Kwa hakika alisema katika riwaya moja: "Mara nyengine Izaar yangu hushuka chini." Kwahiyo, ni Izaar yake inayoshuka iwapo, kama alivyosema, "Siwi na tahadhari ya kuichunga." Ni wazi yakwamba anapoichunga, hubaki juu ya vifundo vyake vya miguu, lakini inapompwaya, hushuka chini. Al-haafidh Ibn Hajar amepokea yakwamba Ibn Sa'd amepokea riwaya kutoka kwenye njia ya Talha bin 'Abdullaah bin Abdur-Rahmaan bin Abee Bakr, yakwamba 'Aaisha (رضي الله عمها وعنهم) alisema: "Abu Bakr alikuwa ni *Ahnaa* (mwenye mgongo ulioinama), Izaar yake haimshiki; humpwaya kwenye kiuno chake." Vilevile al-Haafidh akapokea riwaya nyengine kutoka katika njia ya Qayess Ibn Abee Haazim aliyesema: "Nilimtembelea Abee Bakr nae alikuwa ni mtu mwembamba." [Fat-hul-Baari V.10, Uk. 255].
Watu wenye kutengeneza nguo, surwale n.k ambazo ncha zake za chini zimelingana na Sunnah lakini wanapozivaa huwapwaya na mara nyengine zikashuka chini ya vifundo vya miguu yao, ndio wenye kufanana na hali ya Abu Bakr. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimzingatia Abu Bakr kuwa si miongoni mwa "wenye kuburuta nguo zao kutokana na majivuno," kwa sababu Abu Bakr hakukusudia kuishukisha Izaar yake chini ya vifundo vya miguu yake, na ilikuwa ikiburutika anapokosa kuichunga.
Wale wenye kukusudia kuburuta kutokana na majivuno wametishwa kwa adhabu kali:
Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Allaah hatomwangalia (katika siku ya Kufufuliwa) mtu mwenye kuburuta nguo (nyuma yake) kutokana na majivuno."*
Katika riwaya nyengine, Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Allaah hatomwangalia mtu, katika Siku ya Malipo, mwenye kuburuta Izaar yake kutokana na majivuno na kiburi."*
Juu ya hayo, katika Siku ya Malipo, Allaah hatozungumza au hatomtakasa mtu *Musbil*. Haya yamethibitishwa kwenye hadeeth iliyo swaheeh ambamo Abu Dharr alimopokea kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Kuna watu sampuli tatu ambao Allaah hatozungumza nao katika Siku ya Malipo, wala hatowatizama, wala hatowatakasa, na watakuwa na adhabu kali iumizayo." Akasema (Abu Dharr): Mtume (صلى الله عليه وسلم) akayarudia hayo mara tatu." Abu Dharr akamaka: "Wameanguka wakapotea; ni watu sampuli gani hao, Ewe Mjumbe wa Allaah?". Akajibu Mtume (صلى الله عليه وسلم): "*Mwenye kuburuta nguo zake (Musbil),*

mwenye kuhesabu anachotoa, na muuzaji mali kwa viapo vya urongo."
Kwa hakika Abu Bakr amepata ushuhuda kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba hakuburuta Izaar yake kutokana na kibri. Wenye kufanya Isbaal kwa kukusudia, walipata lini ushuhuda wa kuwatakasa?
Katika tukio jengine, 'Abdullaah Ibn 'Umar (رضي الله عنهما) alipita mbele ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na ikawa Izaar yake imeshuka chini kupita vifundo vya miguu yake, akasema katikia kuelezea tukio hilo: "Siku moja nilipita mbele ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na nguo yangu ikawa imeshuka chini. Akaniambia: 'Abdullaah, hiyo nguo yako ya chini ipandishe juu.' Nikaivuta juu, nae akaniambia tena: 'Endelea kuipandisha zaidi.' Nikazidi kuipandisha na nikaendelea kuipandisha baada ya hapo, mpaka baadhi ya watu wakaanza kuuliza: 'Mpaka wapi?' na hapo ndipo aliposema, 'Mpaka ifike katikati ya miundi."'
Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakunyamaza alipomuona 'Abdullaah Ibn 'Umar akiburuta Izaar yake. Hii yaonyesha yakwamba makatazo ya Isbaal kwa wanaume hayakufungamanishwa na hali ya Makheelah peke yake. 'Abdullaah Ibn 'Umar ni miongoni mwa Maswahaba wakubwa. Waweza kukisia ungelikuwaje msimamo wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) lau kama angeliziona nguo za *ma-Da'ee* (wenye kulingania watu katika njia ya Allaah) wengi wa "kisasa", au hata "mashekhe wetu" kila mmoja akiburuta Jubbah lake, nguo au surwale? Sisi sote twajua yakwamba Ibn 'Umar hachelewi kushikamana na amri za Mtume (صلى الله عليه وسلم). Sasa inachukuwa masaa katika mazungumzo na mihadhara kuwaeleza watu kuhusu amri za Mtume (صلى الله عليه وسلم) na bado utapata watu wakizua mabishano, "Maadamu Isbaal haikufanywa kutokamana na majivuno na kiburi, basi huwa yafaa!" Kwa hakika hayo humtatiza mtu mwenye huruma!

SHUB'HA YA PILI: Mtume (صلى الله عليه وسلم), yeye mwenyewe alikuwa akiburuta nguo zake, sasa ni kwa nini eti kuburuta nguo hairuhusiwi? Watu wenye kushikilia maneno hayo huchukuwa maandiko yafuatayo kuwa ni dalili zao:
Amepokea Abu Bakr (رضي الله عنه):
"Tulikuwa pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم) jua lilipopatwa. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasimama na huku akiburuta joho lake mpaka akaingia msikitini." Na katika riwaya nyengine, Abu Bakr amesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitoka huku akiburuta joho lake mpaka akafika msikitini." Vilevile katika riwaya nyengine itokayo kwa Abu Bakr: "Aliinuka na huku akiburuta joho lake kwa haraka mpaka alipofika msikitini."
Hali nyengine ni pale Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipopiga salamu kwenye swala kabla ya kumalizika swala yenyewe, baada ya raka'ah ya tatu ya swala ya adhuhuri. Mtu mmoja aitwae Al-Khirbaaq, aliyekuwa na mikono mirefu alisimama na kusema: "Jee, swala imefupishwa, Ewe Mjumbe wa Allaah? **Alitoka nje akiwa na hasira na huku akiburuta joho lake na alipokuja kwa watu aliwauliza, 'anasema kweli huyu?'** Wakamjibu: 'Naam, ndio'. Kisha akaikamilisha raka'ah moja, akapiga salamu, kisha akatekeleza sijda mbili (za kusahau), kisha akatoa salamu."
Tukio la tatu limesimuliwa na 'Abdur-Rahmaan Ibn Abee Sa'eed al-Khudaree aliyepokea kutoka kwa babake. Alisema [babake], "Siku ya Jumatatu, mimi na Mtume (صلى الله عليه وسلم) tulikwenda *Qibaa'* mpaka tulipofika makaazi ya Banu Saalim. **Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasimama kwenye mlango wa 'Itbaan na akamwita kwa sauti kubwa. Basi akatoka huku akiburuta nguo yake ya chini.** Juu ya hayo, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: '*Tumemuharakisha huyu bwana.'* 'Itbaan akasema, 'Ewe Mjumbe wa Allaah, ikiwa mtu ameondoka kutoka kwa mkewe kwa haraka bila ya kutokwa na manii, atapaswa kufanya nini (kuhusiana na josho)?' Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): 'Kuwajibika kuoga janaba kunatokana na kutokwa na manii.'"
Hadeeth zote hizo zilizotangulia ni dalili zenye kuunga mkono za rai yakwamba iwapo mtu hakukusudia kushusha nguo yake ya chini, lakini ikatokea yakwamba ameburuta kutokana na hali za dharura, kama vile kuwa kwenye haraka, kuwa na hasira, n.k. Huyu si *Musbil* kwa kusudia. Kwahivyo, anapaswa kukumbushwa, na wala asilaumiwe. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuja akiwa na haraka, na vilevile 'Itbaan. Ruhusa nyengine ni kutokana na haja fulani ya kidharura. Kwa mfano, ikiwa mtu ana kidonda kwenye kisigino chake, anaruhusiwa kukifunika kwa kurefusha nguo yake ya chini iwapo hana njia yoyote nyengine ya kukiziba kidonda chake hicho.

SHUB'HA YA TATU: Imepokewa katika Musannaf ya Ibn Abee Shaybah kwa silsila iliyo swaheeh yakwamba Abdullaah Ibn Mas'ud (رضي الله عنه) "alikuwa akiburuta nguo yake ya chini; na alipoulizwa kuhusu suala hilo alisema: 'Mimi nina miundi membamba sana'."
1. AL-Haafidh Ibn Hajar akaijibu hoja hiyo kwa kusema: "Hii inaashiriya yakwamba aliirefusha kuliko ilivyopendekezwa, ambapo ni katikati ya miundi. Si sawa kutuhumu yakwamba aliiwacha ishuke chini ya vifundo vya miguu kama ilivyoashiriwa na jawabu lake: 'Mimi nina miundi membamba sana.' Kwa kweli, Abdullaah Ibn Mas'ud (رضي الله عنه) amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alichukia mambo kumi." Akayataja na miongoni mwayo ni "Kuburuta Izaar (kupita chini ya vifundo vya miguu). Haya yalipokewa na Imaam Ahmad katika Musnad yake, V.6, Uk. 103-104, hadeeth # 4179. Msahihishaji, Ahmad Shaakir (رحمه الله) amesema: "Isnaad yake ni swaheeh." hili linaunga mkono msimamo wa al-Haafidh yakwamba nguo ya "Isbaal" ya Abdullaah Ibn Mas'ud ilikuwa ni nyongeza iliyopita katikati ya miundi yake na wala haikupita vifundo vya miguu yake.
Kwa hakika Ibn Mas'ud hawezi kupinga msimamo alokuwa nao Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuhusiana na Isbaal.
Vilevile pana uwezekano yakwamba hakuwa na habari kuhusu kisa cha 'Amr bin Zaraarah, na Allaah Ndiye Mjuzi zaidi.
Amepokea Abu Umaamah, "Tulipokuwa pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم) , 'Amr bin Zaraarah al-Answaari alitufuata, nae alikuwa amevaa joho na Izaar yenye kuburutika. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaanza kuishikilia nguo yake upande mmoja, akijidhalilisha kwa Allaah na huku akisema: 'Mimi ni mja wako, mtoto wa mja wako wa kiume, mtoto wa mja wako wa kike,' mpaka 'Amr akayasikiya hayo. Juu ya hayo akasema: **'Ewe Mjumbe wa Allaah! Mimi ni mtu mwenye miundi membamba sana.'** Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Ewe 'Amr! Allaah ameumba kila kitu kwa ukamilifu; Ewe 'Amr! Allaah hampendi mtu Musbil."
2. Riwaya kumuhusu Ibn Mas'ud ni katika kigawanyo cha Mawqoof, inayopingwa na riwaya nyingi zilizo Marfoo'. Kwa hakika, Marfoo' hupewa kipaumbele kuliko Mawqoof. Ushahidi unapatikana kutokana na yaliyothibitishwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم).

[ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO]